# *Pitio la Kitabu*[1] (Irmtraud Herms)

**Ruth Mfumbwa Besha**

## *A Study of Tense and Aspect in Shambala.* Berlin: Reimer 1989. 339 pp. (*Language and Dialect Studies in East Africa.* Vol. 10).

Ni jambo la kufurahisha sana kwamba tasnifu ya PH.D. ya Bi. Ruth M. Besha ambaye ni mtaalamu wa lugha kutoka Tanzania, ilichapwa. Aliiwasilisha tasnifu hii katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mnamo mwaka 1985. Kwani kazi yake haitawafaa wataalamu tu wanaoshughulikia lugha za kibantu (ambazo Kishambala = Kishambaa = Kisambaa, kinachosemwa Kaskazini-Mashariki mwa Tanzania ni mojawapo ya lugha hizo) bali watu wote wanaovutiwa na uhusiano baina ya njeo (wakati; tense) na hali (aspect) ya vitenzi.

Sura ya kwanza ya kitabu hiki ni utangulizi katika nchi ya Washambaa (Shambalai), historia na lugha yao. Kwa mara ya kwanza mwandishi anachunguza lahaja za Kishambaa akitambua lahaja kuu tatu: Lushoto, Mlalo na Korogwe. Anaeleza pia athari ya lugha ya Kiswahili kwa fonolojia, sarufi na msamiati wa Kishambaa, kwani Kiswahili kinakuwa lugha kuu mijini, hasa miongoni mwa vijana, kutokana na mawasiliano, vyombo vya habari, elimu, biashara, uhamiaji mijini. Washambaa wengi hutumia lugha mbili.

Mwandishi ambaye ni mzawa wa lugha ya Kishambaa (lahaja ya Lushoto) aliweza kutumia ndugu zake kama watoa taarifa kuhusu lugha yao. Walimsaidia pia kukusanya data - habari za aina mbalimbali na mazungumzo kuhusu mada za kila siku. Wazee walipenda kueleza hasa kuhusu historia, utamaduni, mila na desturi za kabila lao, ambapo vijana walipendelea kuzungumzia siasa, uchumi na elimu wakiingiza maneno mengi ya Kiswahili. Mwandishi alirekodi pia mazungumzo kuhusu habari za mtaa au kijiji (kwa mfano ugonjwa wa mtoto fulani, arusi ya mtu fulani, vifo, hali ya hewa) bila ya yeye mwenyewe kuonwa.

Wasaidizi na watoa habari zaidi ya 100 wenye umri wa miaka 15 - 90 walishiriki katika ukusanyaji wa data kati ya 1972 - 1981. Wengi wao

[1]Kifupisho cha mapitio haya yalichapishwa kwa Kijerumani katika jarida la "Zeitschrift fuer Dialektologie und Linguistik", LVIII (1991), uk. 123.

walikuwa wakulima, kwani wao ndio waliotumia lugha ya Kishambaa katika maisha yao ya kila siku. Hivyo msingi wa utafiti ni lugha inayozungumzwa (spoken language) - hii ni muhimu pia kwa sababu Kishambaa ni lugha yenye toni.

Sura ya pili inatoa maelezo kuhusu sarufi ya Kishambaa. Kwa vile kumeelezwa vizuri fonolojia, mfumo wa toni, mofolojia (sarufi maumbo - akitilia mkazo vitenzi) na sintaksi (sarufi miundo), msomaji wa kitabu hiki anaweza kufuata vizuri maelezo na mifano, hata ikiwa hajui lugha ya Kishambaa.

Vipo vitabu kadhaa vya sarufi ya Kishambaa vilivyoandikwa na wamisionari wa kilutheri kutoka Ujerumani mwisho wa karne ya 19 na mwanzo wa karne ya 20. Kitabu kilicho kamili zaidi ni kile cha Roehl[2] kilichotumiwa na R. Besha pia.

Katika sura ya 3 na 4 mwandishi anajadili kinagaubaga kazi za isimu zihusuzo njeo na hali za vitenzi, kwa kutumia nadharia ya H. Reichenbach[3], aliyetofautisha "nukta tatu za wakati" (three time points), yaani muda wa kutamka (the point of speech), muda wa tukio (the point of the event) na muda wa marejeo (the point of reference). Chanzo cha utafiti wa R. Besha ni sentensi, lakini anazingatia pia muktadha. Anafasili njeo na hali ifuatavyo: "Tense is the grammatical encoding of temporal reference in language" (uk. 148); "aspects are different ways of viewing the internal temporal constituency of a situation" (kufuatana na Bernard Comrie[4], uk.164).

Kuhusu njeo, ilidhaniwa kwamba pia lugha ya Kishambaa (kama kila lugha yoyote ile) ina njia za kisarufi za kutofautisha kati ya matukio ya wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao; na kuhusu hali (aspect) uliangaliwa mkinzano kati ya hali timilifu / isiyo timilifu na hali mazoea / isiyo mazoea (opposition completive / non-completive, habitual / non-habitual). Nafasi ya mofimu ya njeo / hali / dhamira (mood) inaweza kuchukuliwa na mojawapo kati ya hizo au na mchanganyo mbalimbali (different combinations, uk.64).

Kanuni ya kinadharia iliyofuatwa na R. Besha katika uchambuzi wake ni kwamba kila mofimu iliyotambuliwa iwe na maana moja. Njia iliyotumiwa ni "jaribio la vielezi", yaani kielezi kipi kinaweza kutumiwa pamoja na kiambishi fulani katika sentensi.

---

[2]K.Roehl (1911): Versuch einer systematischen Grammatik der Schambala-Sprache. Hamburg.

[3]H. Reichenbach (1947): Elements of Symbolic Logic. New York.

[4]B. Comrie (1976): Aspect. Cambridge.

Kwenye sura ya 5 na 6 kuna utafiti wenyewe kuhusu njeo na hali za vitenzi katika Kishambaa (lahaja ya Lushoto). Mwandishi amechambua mofimu (anatumia istilahi "marker") zipi ni za njeo, hali na kategoria nyingine za kisarufi (uchunguzi zaidi unahitajika kuhusu dhamira "mood"). Matokeo yake ni:

1) Kuna mofimu tano zinazoashiria *wakati uliopita*: -te-, -iye, -za-, -a-, -na-, -aa-. Mofimu

-iye (allomorphs -e na -ize) ni kiambishi tamati. R. Besha amechambua mofimu zipi zinaweza kutokea katika sentansi gani; kwa mfano katika maswali ya aina ya "wh-" (wh-type questions) kunaweza kutumiwa mofimu -iye na -a-. Amezipanga mofimu hizo kufuatana na umbali au ukaribu na muda wa kutamka (speech time, ST): -aa- ← -a- ← -za- ← -iye ← -te- ← ST.

| | |
|---|---|
| -te- | - Near Past, Independent, Indefinite |
| -iye | - Near Past, Dependent, Definite |
| -a- | - Distant Past, Dependent, Definite |
| -aa- (high/low tone) | - Distant Past, Independent, Indefinite (uk. 191) |

Mofimu -za- ina tatizo, kwa sababu upande mmoja inafanana na -iye, upande mwingine inaashiria matukio yaliyotimia (matilifu) na hivyo inafanana na *perfective aspect*. Na mofimu -za- tu inaweza kutokea mwanzo wa mazungumzo.

2) Kuna mofimu tatu zinazoashiria *wakati uliopo*:
O (zero, dependent present), -ta- (simple present) na -aa- (*progressive present, with low or high tone depending on the tone of the preceding linguistic form)*. Mofimu hizo haziwezi kutokea pamoja na vielezi vya wakati uliopita na vinaashiria matukio yanayotukia wakati mmoja na muda wa kutamka (ST).
3) Mofimu zinazoashiria *wakati ujao* ni viambishi awali ne- (near future, definite) na nee- (distant future, non-definite), ambapo kitenzi kinaishia na -e (sawa na dhamira tegemezi / dhamira ya kutarajia), kwa mfano:

   Ne - ti - dik - e maboko. Tutapika ndizi.
   fut - tu - pik - e ndizi
4) Mofimu za *hali (aspect)* ni:
   -i- (pamoja na mofimu -iye ya wakati uliopita) kwa hali timilifu (perfective) na
   -ke- (pamoja na mofimu O ya wakati uliopo) kwa hali isiyo timilifu (imperfective).

Hali nyingine inaelezwa kwa vielezi mbalimbali.

Kwa kila mofimu Besha ametoa mifano mingi inayothibitisha matokeo yake.

Katika sura ya 7 amechambua kategoria hizo katika mazungumzo / matini tofauti, yaani maelezo ya kihistoria (historical narrative) na maelezo binafsi (personal narrative). Jambo la kuvutia ni jinsi mwandishi anavyojadili matumizi ya mofimu za wakati uliopo katika kusimulia matukio yalliyotukia wakati uliopita.

Sura ya nane inatoa mahitimisho na mapendekezo kwa utafiti wa baadaye, kwa mfano kuhusu aina za vitenzi (*state verbs, process verbs, action verbs n.k.*), kwani si mofimu zote za wakati na hali zinaweza kutokea pamoja na vitenzi vyote (uk.324).

Mwishoni mwa kitabu kuna orodha ndefu za marejeo kuhusu vitabu vya isimu na lugha za kibantu. Kwa bahati mbaya, kusoma kitabu hicho ni kugumu kidogo kwa sababu hakuna orodha ya vifupisho vilivyotumiwa. Utafiti wake ni mchango mkubwa kwa kufafanua suala la njeo na hali katika lugha moja ya kiafrika. Ninapendekeza kitabu hicho kisomwe na wanaisimu wote wasiopenda kuchunguza suala la njeo na hali za vitenzi kupitia miwani ya lugha za Kihindi-Kizungu tu.